RAIA MWEMA
Jumanne, Aprili 5, 2022



Mkurugenzi wa Kiwanda cha Woisso Original Products(WOP), Kenneth Woisso (wa kwanza kulia) akiwa na wawekezaji wa sekta ya ngozi kutoka Misri.

# Zinahitajika jitihada *kuokoa* soko la ngozi

Na Gift Mongi

KUKOSEKANA kwa usimamizi madhubuti wa kisera na kimfumo kunatajwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazosababisha sekta ya ngozi nchini kuendelea kuzorota siku hadi siku jambo linalotishia uhai wa biashara hiyo.

Wadau wa sekta hiyo wanasema kama sio kushamiri kwa vikwazo hivyo, kungeweza kusaidia kuanzishwa kwa viwanda vingi vidogo vidogo ambavyo mbali na kuzalisha ajira pia vingechangia kuimarika kwa soko la ndani la bidhaa za ngozi.

Takwimu zinaeleza kuwa Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikitanguliwa na Afrika Kusini pomoja na Ethiopia.

Kwa mantiki hiyo ni dhahiri uwepo wa idadi kubwa ya mifugo kunaweza kuongeza malighafi yatokanayo na mazao ya mifugo kama nyama, kwato, na hata ngozi ambazo hutumika katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo yaani uzalishaji au utengenezaji bidhaa.

Rajab Mfinanga mkazi wa Kileo wilayani Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ni muuzaji wa ngozi, anasema biashara hiyo kwa sasa inaenda kwa kusuasua.

Anasema kutokana na kukosekana kwa soko lenye uhakika la ndani kwa kiasi kikubwa imechangia wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia njia za panya na kutorosha ngozi nje ya nchi.

"Hakuna soko la uhakika na tozo zimekuwa nyingi ambapo wafanyabiashara badala ya kukusanya ngozi na kuiuza katika soko la ndani, baadhi wasio waaminifu wamekuwa wakitumia njia za panya kuiuza nje ya nchi na kusababisha uhaba wa bidhaa ya ngozi," anaeleza Mfinanga.

Pia anasema kuwa kutokana na hali ilivyo, huenda viwanda vya ndani vinavyozalisha bidhaa za ngozi vikakosa malighafi, kwani ngozi nzuri yote ndio inayopelekwa nje ya nchi kimagendo na inayobaki ni kama makapi ambayo haifai katika uzalishaji.

Mchuuzi wa ngozi wilayani Hai, Japhet Uronu anasema kwa sasa thamani ya ngozi imeshuka na kwamba wapo wafanyabiashara kutoka nchi jirani wanakuja kununua kwa bei nzuri.

> **"Katika sekta ya ngozi kwa sasa zipo changamoto kuu mbili; ambayo ni asilimia 10 ya kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi iliyosindikwa hadi kufikia wett blue. Nyingine ni asilimia 80 kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi ghafi, ambapo kiwango hiki kikipungua huenda biashara hii ikawa sehemu sahihi zaidi ya hapa ilipo."**

"Sasa kuliko mtu akusanye ngozi halafu bado usafiri na kodi mbalimbali anaona ni bora akusanye tu halafu mnunuzi anakuja kuinunua mara moja na usumbufu kunakuwa hakuna," anaeleza Uronu.

Dalali wa ngozi eneo la Bomang'ombe wilayani Hai, Grace Munisi anasema kuwa kinachochangia kuharibika kwa sekta hiyo ni kukosa dira na mwelekeo, hivyo kila mtu kufanya anavyojisikia ili mradi aweze kutengeneza faida.

"Kwa mfano sasa kufanyike jitihada za kuongeza tozo kwa ngozi ambayo inapelekwa nje hapa ni kuwa tozo ikiwa juu hawatapeleka tena maana kutakuwa hakuna faida na ni njia mojawapo katika kuvinusuru viwanda vya ndani," anasema.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Woisso Original Products (WOP), Keneth Woisso anasema kwa siku za karibuni biashara ya ngozi inapita katika wakati mgumu kwani ngozi zimeadimika na nyingi zinasafirishwa nje ya nchi.

Anasema ngozi nzuri yote imekuwa ikisafirishwa nje ya nchi na inayosalia ni mbovu haifai kwa matumizi ya uzalishaji. Woisso anaiomba Serikali kutafuta mbinu za kutatua changamoto hiyo ili kuvinusuru viwanda vya ndani.

"Sisi wazalishaji wa bidhaa za ngozi kwa siku za karibuni tunapitia kipindi kigumu, hakuna malighafi na hata ukipata unazikuta zipo chini ya kiwango yaani hazifai katika uzalishaji wa bidhaa," anasema Woisso na kuongeza:

"Katika sekta ya ngozi kwa sasa zipo changamoto kuu mbili; ambayo ni asilimia 10 ya kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi iliyosindikwa hadi kufikia wett blue. Nyingine ni asilimia 80 kodi ya huduma (export levy) kwenye ngozi ghafi, ambapo kiwango hiki kikipungua huenda biashara hii ikawa sehemu sahihi zaidi ya hapa ilipo."

Anasema kuwa kutokana na kiwango hicho kikubwa cha kodi kumesababisha ngozi nyingi kubaki mikononi mwa wafanyabiashara huku wahitaji wa malighafi wakizikosa.

Mkurugenzi huyo anaeleza kuwa kutokana na hali hiyo ipo haja kwa Serikali kuangalia changamoto hizo kwa undani na kutoa suluhisho ili kuweza kudhibiti baadhi ya wafanyabiashara kuingiza au kuuza ngozi kwa njia ya magendo.

Kuhusiana na hali ya soko la bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani, anasema tayari wananchi wamehamasika kununua bidhaa zinazozalishwa nchini tofauti na kipindi cha nyuma, ambapo bidhaa za nje ndio zilikuwa zinapewa kipaumbele.

Anasema kwa sasa ubunifu umekuwa ni mkubwa jambo ambalo limechangia bidhaa za ndani kuaminiwa, na anatolea mfano wa viatu vya ngozi wanavyozalisha.

"Tunatengeneza viatu vya majeshi, kwa sasa hawaagizi tena nje ya nchi hii ni fursa mpya katika kukuza soko la ndani na kukuza sekta ya ngozi nchini kwa ujumla wake na hali inaelekea kuwa nzuri," anabainisha Woisso.

Pia anasema kuwa kiwanda cha WOP katika kuunga mkono jitihada za Serikali kuelekea uchumi wa viwanda wamejidhatiti kutengeneza bidhaa zenye ubora wa kimataifa ili kukuza soko la bidhaa za ngozi ndani na nje ya nchi.

Scanned with CamScanner

special focus on adolescent girls to

Framework (UNSDCF) 2022-2027"

THE GUARDIAN Page 4

# * Livestock, Fisheries ministry spent 300bn/- in last 5 years treating animal diseases - PS

By Francis Kajubi

THE Ministry of Livestock and Fisheries had spent almost 300bn/- in the last five years to treat livestock diseases in order to bridge the knowledge gap between pastoralists and veterinary officers on livestock emerging epidemic diseases.

The ministry's Permanent Secretary Tixson Nzunda (Livestock) said in Dar es Salaam last Friday at a graduation ceremony of 25 veterinary officers from different regions of the country who had pursued a four months building capacity training programme.

Dubbed 'In-Service Applied Veterinary Epidemiology Training (ISAVET), the programme is intended at grooming veterinary officers at the district level on detecting and acting on emerging livestock epidemic diseases.

"Almost 70 percent of epidemic diseases from humans to livestock and vice versa are yet to be fully controlled. The ministry had spent between 250bn/- and 300bn/- in treating livestock epidemic diseases that can be prevented from occurrence if veterinary officers could properly link themselves to pastoralists by educating them on detection of the diseases and urgent treatments," said Nzunda.

According to him, if the disease knowledge gap between pastoralists and veterinary officers is well bridged, such money could be used in other areas of the ministry.

According to him, the ministry is preparing a 1.95trn/- strategic plan starting with the 2022/23 financial year that targets and transforms the livestock sector to make it more productive through resource mobilization and make the sector offer a vast amount of opportunities to all players.

The plan, he said, is being purposely framed at making the livestock sector a leader in offering employment opportunities in the country.

"I would also like to encourage veterinary officers to adopt the habit of drafting proposals that will convince the ministry to provide their districts or villages with funds for different programmes. It is unfortunate that I have visited almost all districts but find veterinary officers without plans of how they will earn extra funds apart from the allocated budgets for their operations," he said.

He called upon the veterinary officers to go and conduct deep research on trans-boundary diseases.

Dr Moses Ole-Neselle, ISAVET Programme Coordinator said that the 25 officers come from local government authority, veterinary laboratories at district and village levels, Livestock Training Agency (LITA), Ngorongoro Conservation Area Authority (NCAA) and mentors from the Zonal Veterinary Centers (ZVC).

"Themed developing skills in the animal health workforce, the programme targets at training 300 veterinary officers by the year 2025. Our training is focused on epidemiological diseases detection and surveillance, field investigation and response," he said.

He said that the programme is being funded by the USAID and coordinated by the Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO).

Dr Nyabenyi Tipo, FAO Country Representative, said that among other aspects, the organization is focused on livestock welfare that includes disease and researches for better health of humans and livestock.

"This is part of ensuring there is global health security. In this country we know that many communities rely on the livestock sector for their livelihoods this ISAVET programme is critical," said Dr Tipo.

Scanned with CamScanner

# Mwigulu aomba sapoti wadau sekta ya mifugo

Benny Mwalpaja, DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba, ametoa rai kwa wadau wa sekta ya mifugo nchini kuisaidia serikali kutimiza nia yake ya kuimarisha uzalishaji wa nyama na maziwa ili kuongeza tija na kukuza uchumi wa nchi na maendeleo ya watu.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo jijini Dodoma, alipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, wataalamu kutoka wizara hiyo na Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na wazalishaji binafsi katika sekta za maziwa na nyama nchini.

Alisisitiza kuwa sekta ya mifugo itakuwa na mchango mkubwa katika kukuza kipato cha wananchi hususan vijana, lakini itaongeza mapato ya nchi kwa kuzalisha bidhaa za nyama na maziwa zitakazouzwa ndani na nje ya nchi hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni.

Aliwataka wadau hao kuwa walimu wa kuwaongoza na kuwafundisha vijana namna ya kuzalisha mifugo bora kwa ajili ya nyama na maziwa na kwa kuwa wana mtandao wa masoko, ni rahisi kwa wafugaji kupata maeneo ya kuuza mazao yao.

Dk. Nchemba, alitoa wito pia kwa vijana na wawekezaji kuchangamkia fursa zinazopatikana katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili wajipatie ajira katika sekta hizo muhimu badala ya kuwaachia wazee peke yao kujihusisha na masuala ya kilimo na mifugo na kuahidi kuwa serikali iko tayari kuwawezesha maeneo na mitaji.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliwahakikishia wadau hao wanaomiliki kampuni na viwanda vya kusindika nyama na maziwa kwamba serikali iko tayari kushirikiana nao kuboresha sekta ya mifugo ili ilete tija nchini.

Aidha, alisema kuwa fedha zitakazoongezwa na serikali katika Bajeti Kuu ya Mwaka 2022/2023 katika Wizara yake, zitaelekezwa kwenye maeneo yenye kuongeza uzalishaji ili kukuza ajira kwa vijana pamoja na kuzalisha mazao yatakayokuza mauzo nje ya nchi.

Kwa upande wao, wadau wa sekta ya mifugo walioshiriki kikao hicho, wameishauri serikali kukuza sekta ya mifugo kwa kuwekeza kwenye masuala ya vipaumbele ikiwamo uhimilishaji, kuongeza huduma za ugani, afya ya mifugo na kujenga miundombinu ya kuchakata bidhaa za mifugo na kutafuta masoko ya uhakika.

Scanned with CamScanner

# Wadau mifugo waelezwa kusaidia serikali kuimarisha uzalishaji wa nyama, maziwa

**BENNY MWAIPAJA**, *Dodoma*

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigul Nchemba, ametoa rai kwa wadau wa sekta y mifugo nchini kusaidia serikali kutimiza nia yak ya kuimarisha uzalishaji wa nyama na maziw ili kuongeza tija na kukuza uchumi wa nchi n maendeleo ya watu.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo jijini Dodom alipokutana na Waziri wa Mifugo na Uvuv Mashimba Ndaki, wataalamu kutoka wizara hiyo n Wizara ya Fedha na Mipango na wazalishaji binaf katika sekta za maziwa na nyama nchini.

Alisisitiza kuwa sekta ya mifugo itakuwa n mchango mkubwa katika kukuza kipato ch wananchi hususan vijana, pia itaongeza mapat ya nchi kwa kuzalisha bidhaa za nyama na maziw zitakazouzwa ndani na nje ya nchi, hivyo kuongez upatikanaji wa fedha za kigeni.

Waziri Nchemba ametaka wadau hao kuw walimu wa kuwaongoza na kuwafundisha vijan namna ya kuzalisha mifugo bora kwa ajili ya nyam na maziwa na kwa sababu wana mtandao w masoko, ni rahisi kwa wafugaji kupata maeneo y kuuza mazao yao.

Aliwataka vijana na wawekezaji kuchangamka fursa zinazopatikana katika sekta za kilimo, mifug na uvuvi ili wajipatie ajira katika sekta hizo muhim badala ya kuwaachia wazee peke yao kujihusisha n masuala ya kilimo na mifugo na kuahidi serikali ip tayari kuwawezesha maeneo na mitaji.

Naye, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ndak aliwahakikisha wadau hao wanaomiliki kampun na viwanda vya kusindika nyama na maziwa kuw serikali ipo tayari kushirikiana nao kuboresha sekt ya mifugo ili ilete tija nchini.

Alisema fedha zitakazoongezwa na serika

**Waongozeni na kuwafundisha vijana namna ya kuzalisha mifugo bora kwa ajili ya nyama na maziwa kwa sababu mna mtandao wa masoko, ni rahisi kwa wafugaji kupata maeneo ya kuuza mazao yao.**

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba

katika bajeti kuu ya mwaka 2022/2023 katika wizara yake, zitaelekezwa katika maeneo yenye kuongeza uzalishaji ili kukuza ajira kwa vijana na kuzalisha mazao yatakayokuza mauzo nje ya nchi.

Kwa upande wao, wadau wa sekta ya mifugo walioshiriki kikao hicho, walishauri serikali kukuza sekta ya mifugo kwa kuwekeza katika masuala ya vipaumbele ikiwemo uhimilishaji, kuongeza huduma za ugani, afya ya mifugo na kujenga miundombinu ya kuchakata bidhaa za mifugo na kutafuta masoko.

Pia, waliiomba serikali kupitia upya masuala a tozo na kodi kwenye sekta ya mifugo na kuzipunguza ili kuchochea uzalishaji wa sekta hiyo na kupunguza gharama za uzalishaji mbazo zitafanya sekta hiyo kushindana katika oko na kutoa bei nzuri kwa wananchi.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Rais amia Suluhu Hassan, alimwelekeza Dk. chemba kuongeza bajeti ya Mifugo, Uvuvi na limo, ili sekta hizo muhimu ziboreshwe na changia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Scanned with CamScanner

kikongwe, kitaendelea kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya mkoa, ili upae kimaendeleo.

RAIA MWEMA.

# Ukosefu wa samaki waibua imani potofu

**Na Ibrahim Yassin, Songwe**

**UHABA** wa samaki katika Ziwa Rukwa wilayani umetajwa kusababishwa na imani, kwamba baadhi ya wanawake kuvua wakiwa kwenye siku zao.

Imeelezwa, kuwa mwanamke akiwa katika siku zake za mwezi hatakiwi kuvua samaki kwani inasababisha mikosi inayokimbiza samaki.

Hayo yalibainika juzi, baada ya gazeti hili kufika eneo la Ziwa hilo na kushuhudia samaki wachache wenye vichwa vikubwa na kusababisha wavuvi kujenga imani hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Joshua Michael mvuvi wa Mbangala, alidai kuwa kutokana na uhaba wa kitoweo, akina mama wamejiingiza kwenye uvuvi, baadhi yao wakifanya hivyo huku wakiwa kwenye siku zao.

Maria Mayala wa Udinde, alidai kuwa wanalazimika kuvua samaki ili wapate kitoweo, hivyo wakikatazwa kwa sababu hiyo, watakosa, akidai haoni kama jambo hilo lina ukweli ila anachojua waume zao hawataki nao wajiingize kwenye uvuvi.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya, Joel John alisema kuadimika kwa samaki Ziwa Rukwa hata yeye ameambiwa imetokana na hali hiyo, lakini si kweli.

Alisema ni kweli samaki wametoweka, sababu kuu ni mabadiliko ya tabianchi, mvua kunyesha kupita kiasi hali iliyoondoa mazalia ya samaki, baada ya maeneo yenye vichaka kuondolewa na maji, huku samaki wakikosa maeneo ya kutagia mayai.

John alisema mvua inapokuwa nyingi kupita kiasi, huondoa chakula chenye virutubisho, ambapo pia samaki kukosa rutuba na kuzaliwa wakiwa na vichwa vikubwa, ambapo hawaelewi idadi ya samaki mpaka wafanye sensa.

Sababu nyingine kwa mujibu wa John, ni idadi kubwa ya wavuvi kuliko wingi wa samaki na kwamba wanahitaji taasisi ya utafiti itafiti na kupandikiza samaki wapya watakaoishi ziwani humo na wakizaliana wakidhi mahitaji ya walaji.

Scanned with CamScanner